JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA MATOKEO YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE NA KIDATO CHA PILI ILIYOFANYIKA OKTOBA/NOVEMBA, 2024

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MTENDAJI**
**TAREHE : 04 JANUARI, 2025**

**TAARIFA YA MATOKEO YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE NA KIDATO CHA PILI ILIYOFANYIKA OKTOBA/NOVEMBA, 2024**

## 1.0 UTANGULIZI

Katika Mkutano wake wa **163** uliofanyika tarehe **03 Januari, 2025** katika ofisi za Baraza la Mitihani la Tanzania zilizopo Dar es Salaam, Baraza la Mitihani la Tanzania liliidhinisha kutangazwa rasmi kwa matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili iliyofanyika mwezi Oktoba/Novemba, 2024.

## 2.0 USAJILI NA MAHUDHURIO

### 2.1 Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne

Jumla ya wanafunzi **1,633,279** walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne wakiwemo Wasichana **839,515** sawa na asilimia **51.40** na Wavulana **793,764** sawa na asilimia **48.60**. Kati ya wanafunzi waliosajiliwa, wanafunzi **1,530,911** walifanya Upimaji, wakiwemo Wasichana **797,691** (**95.02%**) na Wavulana **733,220** (**92.37%**). Wanafunzi **102,368** (**6.27%**) hawakufanya Upimaji.

### 2.2 Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili

#### (a) Wanafunzi Wote

Jumla ya wanafunzi **879,352** walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili wakiwemo Wasichana **476,244** (**54.16%**) na Wavulana **403,108** (**45.84%**). Kati ya wanafunzi **879,352** waliosajiliwa, wanafunzi wa Shule walikuwa **869,743** na wanafunzi wa Kujitegemea walikuwa **9,609**.

#### (b) Wanafunzi wa Shule

Kati ya wanafunzi **869,743** wa Shule waliosajiliwa, wanafunzi **797,564** sawa na asilimia **91.70** walifanya upimaji ambapo Wasichana walikuwa **437,833** (**93.09%**) na Wavulana **359,731** (**90.07%**). Wanafunzi **72,179** sawa na asilimia **8.30** hawakufanya Upimaji.

(c) **Wanafunzi wa Kujitegemea**

Kati ya wanafunzi **9,609** wa Kujitegemea waliosajiliwa, wanafunzi **7,527** sawa na asilimia **78.33** walifanya Upimaji na wanafunzi **2,082** sawa na asilimia **21.67** hawakufanya Upimaji.

## 3.0 MATOKEO YA UPIMAJI

### 3.1 Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne

#### 3.1.1 Ufaulu wa Ujumla

Jumla ya wanafunzi **1,320,227** kati ya **1,530,805** wenye matokeo sawa na asilimia **86.24** wamefaulu kuendelea na Darasa la Tano mwaka 2025 kwa kupata Madaraja ya **A**, **B**, **C** na **D**. Mwaka 2023 Wanafunzi waliofaulu walikuwa **1,287,934** sawa na asilimia **83.34**. Hivyo, kumekuwa na **ongezeko** la ufaulu kwa asilimia **2.90** kwa wanafunzi waliopata fursa ya kuendelea na Darasa la Tano ikilinganishwa na mwaka 2023.

Kati ya wanafunzi waliofaulu kuendelea na Darasa la Tano, Wasichana ni **699,901** sawa na asilimia **87.75** na Wavulana ni **620,326** sawa na asilimia **84.61**. Takwimu zinaonesha kuwa, Wasichana wamefaulu zaidi ikilinganishwa na Wavulana. Mchanganuo wa ufaulu wa Jumla wa wanafunzi umeainishwa katika **Jedwali Na. 1**.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Jumla wa Wanafunzi**

| Mwaka | Jinsi | Wenye Matokeo | Waliofaulu Gredi (A-D) | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi | % |
| 2023 | Ke | 803,513 | 681,259 | 84.79 |
| | Me | 741,817 | 606,675 | 81.78 |
| | Jumla | 1,545,330 | 1,287,934 | 83.34 |
| 2024 | Ke | 797,642 | 699,901 | 87.75 |
| | Me | 733,163 | 620,326 | 84.61 |
| | Jumla | 1,530,805 | 1,320,227 | 86.24 |

### 3.1.2 Ubora wa Ufaulu

Wanafunzi wa Shule waliopata Madaraja ya **A - C** ambayo ni ya ubora wa ufaulu ni **931,468** sawa na asilimia **60.85**. Mwaka 2023 wanafunzi waliopata ufaulu wa Madaraja **A - C** walikuwa **809,379** sawa na asilimia **52.38**. Hivyo, ubora wa ufaulu **umeongezeka** kwa asilimia **8.47** ikilinganishwa na mwaka 2023.

Kuna uwiano mzuri wa ubora wa ufaulu kati ya Wavulana na Wasichana, ambapo Wavulana waliopata Madaraja ya **A - C** ni **445,673** (**60.79%**) na Wasichana waliopata ni **485,795** (**60.90%**). Mchanganuo wa ufaulu katika Madaraja mbalimbali umeainishwa katika Jedwali Na.**2**.

**Jedwali Na. 2: Ufaulu wa Jumla Kimadaraja**

| Daraja | Mwaka | Wavulana | | Wasichana | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| A | 2023 | 21,869 | 2.95 | 20,219 | 2.52 | 42,088 | 2.72 |
| | 2024 | 40,920 | 5.58 | 37,078 | 4.65 | 77,998 | 5.10 |
| B | 2023 | 102,860 | 13.87 | 102,134 | 12.71 | 204,994 | 13.27 |
| | 2024 | 150,236 | 20.49 | 145,529 | 18.24 | 295,765 | 19.32 |
| C | 2023 | 264,969 | 35.72 | 297,328 | 37.00 | 562,297 | 36.39 |
| | 2024 | 254,517 | 34.71 | 303,188 | 38.01 | 557,708 | 36.43 |
| A-C | 2023 | 389,698 | 52.53 | 419,681 | 52.23 | 809,379 | 52.38 |
| | 2024 | 445,673 | 60.79 | 485,795 | 60.90 | 931,468 | 60.85 |
| D | 2023 | 216,977 | 29.25 | 261,578 | 32.55 | 478,555 | 30.97 |
| | 2024 | 174,653 | 23.82 | 214,106 | 26.84 | 388,759 | 25.40 |
| A-D | 2023 | 606,675 | 81.78 | 681,259 | 84.79 | 1,287,934 | 83.34 |
| | 2024 | 620,326 | 84.61 | 699,901 | 87.75 | 1,320,227 | 86.24 |
| E | 2023 | 135,142 | 18.22 | 122,254 | 15.21 | 257,396 | 16.66 |
| | 2024 | 112,837 | 15.39 | 97,741 | 12.25 | 210,578 | 13.76 |

### 3.1.3 Ufaulu wa Shule katika Makundi ya Umahiri

Idadi ya shule katika makundi ya Umahiri inaonesha kuwa, kati ya shule zote **20,036**, shule **12,865** (**64.20%)** zimepata wastani wa Daraja la **A-C,** ikiwa ni ongezeko la asilimia **10.75** ikilinganishwa na mwaka 2023. Aidha, idadi ya shule **19,839** sawa na asilimia **99.01** zimepata wastani wa Daraja la **A-D**. Mchanganuo wa idadi ya shule katika Makundi ya Umahiri umebainishwa katika Jedwali Na. **2**.

**Jedwali Na. 2: Idadi ya Shule katika Makundi ya Umahiri kwa Mwaka 2024 ikilinganishwa na Mwaka 2023**

| Daraja | 2024 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | % | Idadi | % |
| A [241-300] | 1,139 | 5.68 | 585 | 3.04 |
| B [181-240] | 2,090 | 10.43 | 1,692 | 8.78 |
| C [121-180] | 9,636 | 48.09 | 8,020 | 41.63 |
| D [61-120] | 6,974 | 34.81 | 8,642 | 44.86 |
| E [0-60] | 197 | 0.98 | 325 | 1.69 |
| **Jumla** | **20,036** | **100** | **19,264** | **100** |

## 3.2 Ufaulu wa Wanafunzi Kimasomo

### (a) Masomo ya Lugha

Ufaulu wa somo la **Kiswahili** ni asilimia **84.52** na ufaulu wa somo la **English Language** ni asilimia **68.86** ambapo katika somo la **Kiswahili** umepanda kwa asilimia **0.37** na somo la **English Language** umeshuka kwa asilimia **3.68** ikilinganishwa na mwaka 2023.

### (b) Masomo ya Sayansi Jamii

Ufaulu wa somo la **Maarifa ya Jamii** na **Uraia na Maadili** ni mzuri ambapo ufaulu wa somo la **Maarifa ya Jamii** ni asilimia **89.80** na katika somo la **Uraia na Maadili** ni asilimia **86.35**.

### (c) Masomo ya Sayansi na Hisabati

Ufaulu wa somo la **Sayansi na Teknolojia** ni asilimia **87.87** na somo la **Hisabati** ni asilimia **71.40** ambapo katika somo la **Sayansi na Teknolojia** umeongezeka kwa asilimia **1.01** na somo la **Hisabati** umeongezeka kwa asilimia **17.40** ikilinganishwa na mwaka 2023. Aidha, Wasichana wamefaulu vizuri zaidi katika somo la Sayansi na Teknolojia, lakini Wavulana wamekuwa bora katika somo la Hisabati.

Mchanganuo wa ufaulu wa wanafunzi katika masomo mbalimbali umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu kwa Wanafunzi katika Masomo Mbalimbali**

| Somo | Mwaka | Idadi | %Waliopata A [41-50] | %Waliopata A hadi B [31-50] | %Waliopata A hadi C [21-50] | % Waliopata A hadi D [11-50] | | | %Waliopata E [0-10] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Was. | Wav. | Jumla | |
| Kiswahili | 2023 | 1,544,579 | 20.83 | 43.44 | 66.63 | 85.91 | 82.24 | 84.15 | 15.85 |
| | 2024 | 1,530,510 | 23.99 | 47.41 | 68.87 | 87.01 | 81.81 | 84.52 | 15.48 |
| English Language | 2023 | 1,544,931 | 4.40 | 7.75 | 23.94 | 75.04 | 69.84 | 72.54 | 27.46 |
| | 2024 | 1,530,093 | 5.69 | 8.01 | 18.49 | 71.05 | 66.48 | 68.86 | 31.14 |
| Maarifa ya Jamii | 2023 | 1,544,782 | 2.98 | 18.01 | 54.98 | 87.69 | 85.74 | 86.75 | 13.25 |
| | 2024 | 1,530,278 | 7.31 | 26.07 | 58.79 | 90.56 | 88.97 | 89.80 | 10.20 |
| Hisabati | 2023 | 1,544,799 | 2.14 | 7.42 | 23.28 | 52.70 | 55.40 | 54.00 | 46.00 |
| | 2024 | 1,530,456 | 3.38 | 17.80 | 46.19 | 71.14 | 71.69 | 71.40 | 28.60 |
| Sayansi na Teknolojia | 2023 | 1,544,860 | 2.58 | 18.22 | 54.62 | 87.64 | 86.01 | 86.86 | 13.14 |
| | 2024 | 1,530,273 | 8.98 | 32.75 | 63.11 | 88.32 | 87.38 | 87.87 | 12.13 |
| Uraia na Maadili | 2023 | 1,544,875 | 5.70 | 33.85 | 62.33 | 86.41 | 84.55 | 85.52 | 14.48 |
| | 2024 | 1,530,461 | 9.74 | 41.18 | 70.20 | 87.76 | 84.81 | 86.35 | 13.65 |

## 3.3 Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili

### 3.3.1 Ufaulu wa Ujumla

#### (a) Wanafunzi wa Shule

Jumla ya wanafunzi wa Shule **680,574** kati ya **796,825** wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia **85.41** wamefaulu kuendelea na Kidato cha Tatu ambapo wamepata Madaraja ya **I**, **II**, **III** na **IV**. Mwaka 2023 Wanafunzi waliofaulu walikuwa **592,741** sawa na asilimia **85.31**. Hivyo, ufaulu **umeongezeka** kwa asilimia **0.10**.

Kati ya wanafunzi **680,574** waliofaulu kuendelea na Kidato cha Tatu, Wasichana ni **367,457** sawa na asilimia **83.99** na Wavulana ni **313,117** sawa na asilimia **87.13**. Hivyo, Wavulana wamekuwa na ufaulu bora kuliko Wasichana.

#### (b) Wanafunzi wa Kujitegemea

Wanafunzi wa Kujitegemea waliofaulu upimaji na kupata sifa ya kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne ni **4,205** sawa na asilimia **55.94**. Huu ni mwaka wa kwanza kwa wanafunzi

wa Kujitegemea kutahiniwa upimaji huu. Katika mwaka 2023, wanafunzi wa Kujitegemea **4,238** sawa na asilimia **49.11** walifaulu Mtihani wa Maarifa (QT) na kupata sifa ya kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne. Hivyo, kuna ongezeko la asilimia **6.83** ya wanafunzi waliofaulu na kupata fursa ya kujiandaa kwa Mtihani wa Kidato cha Nne kama watahiniwa wa Kujitegemea ikilinganishwa na mwaka 2023.

Mchanganuo wa ufaulu wa Jumla katika Upimaji wa FTNA 2024 umeainishwa katika Jedwali Na.**4**.

**Jedwali Na. 4: Ufaulu wa Jumla katika Upimaji wa FTNA 2024**

| Aina ya Wanafunzi | Mwaka | Jinsi | Wenye Matokeo | Waliofaulu | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Idadi | % |
| Wa Kujitegemea | 2023 | Ke | - | - | - |
| | | Me | - | - | - |
| | | Jumla | - | - | - |
| | 2024 | Ke | 4,569 | 2,368 | 51.83 |
| | | Me | 2,948 | 1,837 | 62.31 |
| | | Jumla | 7,517 | 4,205 | 55.94 |
| Wa Shule | 2023 | Ke | 376,479 | 314,949 | 83.66 |
| | | Me | 318,290 | 277,792 | 87.28 |
| | | Jumla | 694,769 | 592,741 | 85.31 |
| | 2024 | Ke | 437,478 | 367,457 | 83.99 |
| | | Me | 359,347 | 313,117 | 87.13 |
| | | Jumla | 796,825 | 680,574 | 85.41 |

### 3.3.2 Ubora wa Ufaulu

Ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata wanafunzi wa Shule unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi waliopata ufaulu mzuri wa Madaraja ya **I - III** ni **239,707** sawa na asilimia **30.08**. Mwaka 2023 wanafunzi waliopata ufaulu wa madaraja **I - III** walikuwa **192,633** sawa na asilimia **27.73**. Hivyo, ubora wa ufaulu **umeongezeka** kwa asilimia **2.35** ikilinganishwa na mwaka 2023. Wavulana wana ubora wa ufaulu wa Madaraja ya **I - III** mzuri zaidi ikilinganishwa na Wasichana ambapo Wavulana ni **132,764 (36.95%)** na Wasichana ni **106,943 (24.45%)**. Mchanganuo wa ufaulu katika Madaraja mbalimbali umeainishwa katika **Jedwali Na.5**.

**Jedwali Na. 5: Ufaulu wa Wanafunzi wa Shule Kimadaraja**

| Daraja | Mwaka | Wavulana | | Wasichana | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| I | 2023 | 33,359 | 10.48 | 24,821 | 6.59 | 58,180 | 8.37 |
| | 2024 | 45,155 | 12.57 | 32,617 | 7.46 | 77,772 | 9.76 |
| II | 2023 | 29,359 | 9.22 | 22,635 | 6.01 | 51,994 | 7.48 |
| | 2024 | 35,059 | 9.76 | 27,051 | 6.18 | 62,110 | 7.79 |
| III | 2023 | 44,140 | 13.87 | 38,319 | 10.18 | 82,459 | 11.87 |
| | 2024 | 52,550 | 14.62 | 47,275 | 10.81 | 99,825 | 12.53 |
| I-III | 2023 | 106,858 | 33.57 | 85,775 | 22.78 | 192,633 | 27.73 |
| | 2024 | 132,764 | 36.95 | 106,943 | 24.45 | 239,707 | 30.08 |
| IV | 2023 | 170,934 | 53.70 | 229,174 | 60.87 | 400,108 | 57.59 |
| | 2024 | 180,353 | 50.19 | 260,514 | 59.55 | 440,867 | 55.33 |
| I-IV | 2023 | 277,792 | 87.28 | 314,949 | 83.66 | 592,741 | 85.31 |
| | 2024 | 313,117 | 87.13 | 367,457 | 83.99 | 680,574 | 85.41 |
| 0 | 2023 | 40,498 | 12.72 | 61,530 | 16.34 | 102,028 | 14.69 |
| | 2024 | 46,230 | 12.87 | 70,021 | 16.01 | 116,251 | 14.59 |

### 3.3.3 Ufaulu wa Shule katika Makundi ya Umahiri

Idadi ya shule katika makundi ya Umahiri inaonesha kuwa, kati ya shule zote **5,900** zenye matokeo, shule **1,570** (**26.61%**) zimepata wastani wa Daraja la **A-C** ikiwa ni ongezeko la asilimia **2.46** ikilinganishwa na mwaka 2023. Aidha, idadi ya shule **5,873** sawa na asilimia **99.54** zimepata wastani wa Daraja la **A-D**. Mchanganuo zaidi umebainishwa katika Jedwali Na. **6**.

**Jedwali Na. 6: Idadi ya Shule katika Makundi ya Umahiri kwa Mwaka 2024 ikilinganishwa na Mwaka 2023**

| Daraja | 2024 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | % | Idadi | % |
| A | 155 | 2.63 | 96 | 1.74 |
| B | 556 | 9.42 | 471 | 8.54 |
| C | 859 | 14.56 | 765 | 13.87 |
| D | 4,303 | 72.93 | 4,153 | 75.30 |
| F | 27 | 0.46 | 30 | 0.54 |

### 3.3.4 Ufaulu wa Wanafunzi Kimasomo

#### (a) Masomo ya Sayansi Jamii

Ufaulu wa somo la **History** na **Geography** ni wa wastani ambapo katika somo la **History** ni asilimia **56.37** na katika somo la **Geography** ni asilimia **58.51**. Katika somo la **Civics** ufaulu umeshuka kutoka asilimia **48.27** mwaka 2023 hadi asilimia **33.24** mwaka 2024. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Sayansi Jamii umeoneshwa katika **Jedwali Na. 7**.

**Jedwali Na. 7: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Sayansi Jamii**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Civics | 2023 | 694,373 | 0.72 | 2.96 | 18.19 | 48.27 | 51.73 |
| | 2024 | 796,366 | 0.46 | 2.20 | 13.44 | 33.24 | 66.76 |
| History | 2023 | 694,068 | 2.84 | 6.11 | 19.24 | 50.71 | 49.29 |
| | 2024 | 796,154 | 6.82 | 11.84 | 29.30 | 56.37 | 43.63 |
| Geography | 2023 | 694,237 | 2.43 | 6.40 | 24.66 | 53.78 | 46.22 |
| | 2024 | 796,392 | 6.64 | 13.12 | 33.39 | 58.51 | 41.49 |

#### (b) Masomo ya Lugha

Ufaulu wa somo la **Kiswahili** na **Chinese Language** ni mzuri sana ambapo katika somo la Kiswahili ni asilimia **91.74** na katika somo la **Chinese Language** ni asilimia **90.82**. Masomo ya **Arabic Language** na **French Language** yana ufaulu wa wastani ambapo ufaulu wa masomo hayo ni kati ya asilimia **51.06** hadi **69.07**.

Aidha, katika somo la **English Language** ufaulu umeongezeka kutoka asilimia **68.27** mwaka 2023 hadi asilimia **74.58** mwaka 2024. Mchanganuo wa masomo ya Lugha umeoneshwa katika **Jedwali Na. 8**.

**Jedwali Na. 8: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Lugha**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | 2023 | 694,400 | 4.24 | 14.19 | 64.15 | 95.19 | 4.81 |
| | 2024 | 796,424 | 5.35 | 15.35 | 62.53 | 91.74 | 8.26 |
| English Language | 2023 | 694,321 | 5.10 | 10.52 | 31.48 | 68.27 | 31.73 |
| | 2024 | 796,413 | 7.10 | 13.44 | 38.31 | 74.58 | 25.42 |
| French Language | 2023 | 10,269 | 5.91 | 10.97 | 29.28 | 55.61 | 44.39 |
| | 2024 | 9,809 | 2.24 | 6.86 | 31.62 | 69.07 | 30.93 |
| Arabic Language | 2023 | 2,506 | 3.71 | 8.46 | 27.85 | 48.72 | 51.28 |
| | 2024 | 2,021 | 3.71 | 8.96 | 28.35 | 51.06 | 48.94 |
| Chinese Language | 2023 | 1,921 | 18.32 | 34.31 | 67.52 | 93.39 | 6.61 |
| | 2024 | 1,841 | 8.26 | 17.22 | 60.51 | 90.82 | 9.18 |

(c) **Masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia**

Ufaulu wa masomo ya **Engineering Science**, **Information & Computer Studies** na **Home Economics** ni wa wastani ambao ni kati ya asilimia **51.46** hadi asilimia **62.97**. Masomo ya **Basic Mathematics, Physics**, **Chemistry**, **Agriculture** na **Biology** yana ufaulu ulio chini ya wastani ambao ni kati ya asilimia **18.85** hadi **47.00**.

Takwimu zinaonesha kuwa, ufaulu wa masomo ya **Home Economics**, **Physics**, **Chemistry** na **Additional Mathematics** unazidi kuimarika ambapo kwa mwaka 2024 ufaulu **umeongezeka** kati ya asilimia **3.18** hadi **14.65** ikilinganishwa na mwaka 2023. Aidha, katika somo la **Biology** ufaulu umeshuka kutoka asilimia **55.74** mwaka 2023 hadi asilimia **47.00** mwaka 2024. Mchanganuo wa masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia umeoneshwa katika **Jedwali Na. 9**.

**Jedwali Na. 9: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Sayansi Asilia, Hisabati na Teknolojia**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Physics | 2023 | 691,055 | 0.73 | 1.80 | 7.26 | 19.06 | 80.94 |
| | 2024 | 793,765 | 1.46 | 3.31 | 10.70 | 23.29 | 76.71 |
| Chemistry | 2023 | 694,343 | 1.98 | 4.00 | 12.30 | 28.16 | 71.84 |
| | 2024 | 796,098 | 1.28 | 3.78 | 15.32 | 34.29 | 65.71 |
| Biology | 2023 | 694,013 | 6.05 | 11.07 | 27.91 | 55.74 | 44.26 |
| | 2024 | 796,399 | 3.31 | 6.90 | 21.71 | 47.00 | 53.00 |
| Agriculture | 2023 | 27,022 | 1.22 | 3.40 | 16.26 | 39.24 | 60.76 |
| | 2024 | 28,995 | 0.27 | 1.25 | 10.90 | 34.50 | 65.50 |
| Engineering Science | 2023 | 1,889 | 1.54 | 7.36 | 34.83 | 59.40 | 40.60 |
| | 2024 | 1,712 | 4.56 | 9.52 | 28.62 | 51.46 | 48.54 |
| Information & Computer Studies | 2023 | 14,731 | 4.47 | 13.03 | 41.93 | 67.62 | 32.38 |
| | 2024 | 20,365 | 3.89 | 12.98 | 40.50 | 60.82 | 39.18 |
| Basic Mathematics | 2023 | 694,275 | 4.67 | 7.08 | 13.42 | 21.08 | 78.92 |
| | 2024 | 796,316 | 2.40 | 4.15 | 10.13 | 18.85 | 81.15 |
| Additional Mathematics | 2023 | 441 | 16.78 | 28.12 | 51.70 | 70.29 | 29.71 |
| | 2024 | 392 | 23.47 | 42.09 | 72.19 | 84.95 | 15.05 |
| Home Economics | 2023 | 5,302 | 1.47 | 6.37 | 30.33 | 59.79 | 40.21 |
| | 2024 | 6,052 | 0.28 | 3.06 | 31.96 | 62.97 | 37.03 |

(d) **Masomo ya Biashara**

Ufaulu wa somo la **Book-Keeping** umeendelea kubaki kuwa wa wastani kwa asilimia **51.51** na ufaulu wa somo la **Commerce umeshuka** kutoka asilimia **50.28** mwaka 2023 hadi asilimia **43.77** mwaka 2024. Mchanganuo wa masomo ya Biashara umeoneshwa katika **Jedwali Na. 10**.

**Jedwali Na. 10: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Biashara**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Commerce | 2023 | 70,704 | 3.86 | 9.83 | 29.03 | 50.28 | 49.72 |
| | 2024 | 75,263 | 3.42 | 8.58 | 25.28 | 43.77 | 56.23 |
| Book-Keeping | 2023 | 70,994 | 3.71 | 8.86 | 29.33 | 52.84 | 47.16 |
| | 2024 | 74,829 | 2.55 | 6.54 | 25.60 | 51.51 | 48.49 |

(e) **Masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Ufaulu wa somo la **Fine Art, Theatre Arts** na **Music** ni mzuri ambapo katika somo la **Fine Art** ni asilimia **84.16**, **Theatre Arts** ni asilimia **71.35** na somo la **Music** ni asilimia **80.91**. Somo la **Physical Education** lina ufaulu wa chini ya wastani ambapo ni asilimia **25.24**. Mchanganuo wa masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 11**.

**Jedwali Na. 11: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fine Art | 2023 | 1,496 | 1.07 | 6.89 | 49.87 | 81.89 | 18.11 |
| | 2024 | 2,229 | 0.67 | 4.35 | 44.28 | 84.16 | 15.84 |
| Music | 2023 | 273 | 26.37 | 32.97 | 56.78 | 74.36 | 25.64 |
| | 2024 | 419 | 8.83 | 22.91 | 59.43 | 80.91 | 19.09 |
| Physical Education | 2023 | 7,282 | 0.04 | 0.30 | 6.33 | 27.93 | 72.07 |
| | 2024 | 7,970 | 0.03 | 0.43 | 6.99 | 25.24 | 74.76 |
| Theatre Arts | 2023 | 429 | 0.00 | 1.86 | 20.28 | 48.95 | 51.05 |
| | 2024 | 377 | 3.45 | 14.32 | 41.38 | 71.35 | 28.65 |

(f) **Masomo ya Ufundi**

Masomo yote ya Ufundi yana ufaulu juu ya wastani ambapo somo lenye ufaulu wa juu ni **Building Construction** lenye ufaulu wa asilimia **84.79** likifuatiwa na somo la **Electrical Engineering** lenye ufaulu wa asilimia **83.66**. Aidha somo lenye ufaulu wa chini kabisa ni **Woodwork and Painting Engineering** lenye ufaulu wa asilimia **59.20**. Mchanganuo wa ufaulu wa masomo ya Ufundi umeoneshwa katika **Jedwali Na. 12**.

### Jedwali Na. 12: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Ufundi

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Building Construction | 2023 | 545 | 0.00 | 3.30 | 30.28 | 57.98 | 42.02 |
| | 2024 | 434 | 5.30 | 16.36 | 58.53 | 84.79 | 15.21 |
| Architectural Draughting | 2023 | 526 | 1.52 | 7.22 | 33.84 | 58.56 | 41.44 |
| | 2024 | 416 | 1.44 | 4.57 | 43.27 | 76.20 | 23.80 |
| Civil Engineering Survey | 2023 | 281 | 1.07 | 3.20 | 35.94 | 61.57 | 38.43 |
| | 2024 | 197 | 0.00 | 0.51 | 16.75 | 59.90 | 40.10 |
| Woodwork and Painting Engineering | 2023 | 192 | 0.00 | 0.52 | 34.90 | 63.02 | 36.98 |
| | 2024 | 174 | 0.00 | 0.00 | 10.34 | 59.20 | 40.80 |
| Electrical Engineering | 2023 | 371 | 0.00 | 2.16 | 31.27 | 65.77 | 34.23 |
| | 2024 | 410 | 2.68 | 17.80 | 58.78 | 83.66 | 16.34 |
| Electronics and Communications Engineering | 2023 | 307 | 0.65 | 13.03 | 57.00 | 77.85 | 22.15 |
| | 2024 | 271 | 2.58 | 11.44 | 39.48 | 71.59 | 28.41 |
| Mechanical Engineering | 2023 | 381 | 1.84 | 15.22 | 56.69 | 75.07 | 24.93 |
| | 2024 | 300 | 2.00 | 13.67 | 54.00 | 78.00 | 22.00 |
| Engineering Drawing | 2023 | 431 | 2.78 | 14.39 | 47.33 | 73.55 | 26.45 |
| | 2024 | 344 | 6.40 | 15.99 | 51.16 | 70.06 | 29.94 |

#### (g) Masomo ya Dini

Masomo ya Dini yameonesha mabadiliko makubwa ya ufaulu, somo la **Bible Knowledge** limeongezeka ufaulu kutoka asilimia **84.01** mwaka 2023 hadi asilimia **94.14** mwaka 2024 na somo la **Elimu ya Dini ya Kiislamu** limeongezeka ufaulu kutoka asilimia **68.32** mwaka 2023 hadi **71.41** mwaka 2024. Mchanganuo wa masomo ya Dini umeoneshwa katika **Jedwali Na**. **13**.

### Jedwali Na. 13: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Dini

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bible Knowledge | 2023 | 22,175 | 13.12 | 34.48 | 70.20 | 84.01 | 15.99 |
| | 2024 | 22,851 | 35.20 | 59.94 | 87.32 | 94.14 | 5.86 |
| Elimu ya Dini ya Kiislamu | 2023 | 87,272 | 0.23 | 2.05 | 26.78 | 68.32 | 31.68 |
| | 2024 | 103,871 | 0.76 | 3.66 | 31.11 | 71.41 | 28.59 |

## 4.0 MATOKEO YALIYOFUTWA

Baraza la Mitihani limefuta matokeo yote ya wanafunzi;

(a) **100** waliofanya udanganyifu na **watano** (**05**) waliandika matusi kwenye skripti zao katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne.

(b) **41** waliofanya udanganyifu na **watano** (**05**) waliandika matusi kwenye skripti zao katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili.

Matokeo hayo yamefutwa kwa mujibu wa Kifungu cha **5 (2) (j)** cha sheria ya Baraza la Mitihani sura ya **107** kikisomwa pamoja na Kifungu cha **30(2) (b)** cha Kanuni za Mitihani za mwaka 2016.

## 5.0 KITUO KILICHOFUNGIWA KUWA KITUO CHA MITIHANI YA TAIFA

Baraza la Mitihani la Tanzania limefungia kituo cha S2527 GoodWill S.S. kilichopo mkoa wa Arusha kuwa kituo cha Upimaji na Mitihani ya Taifa kutokana na Mkuu wa Shule na baadhi ya walimu kuthibitika kufanya udanganyifu kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi. Kituo hicho kinafungiwa kwa mujibu wa Kifungu **4**(**8**) cha Kanuni za Mitihani mwaka 2016 hadi hapo Baraza litakapojiridhisha kuwa ni salama kwa uendeshaji wa Upimaji na Mitihani ya Taifa.

## 6.0 PONGEZI ZA BARAZA

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Kamati za Uendeshaji Mitihani za Mikoa na Halmashauri/Manispaa/Jiji, Wakuu wa Shule, Wasimamizi na Wasahihishaji wa Upimaji uliyofanyika Oktoba/Novemba, 2024 kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya katika kutekeleza jukumu la Uendeshaji Upimaji huo. Aidha, Baraza linawapongeza wanafunzi wote waliofanya Upimaji kwa kuwa na utulivu na kuzingatia taratibu za mitihani katika kipindi chote cha Uendeshaji wa Mitihani.

## 7.0 UPATIKANAJI WA MATOKEO

Matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) na Kidato cha Pili (FTNA) iliyofanyika Oktoba/Novemba, 2024 yanapatikana katika tovuti zifuatazo:

- www.necta.go.tz,
- www.moe.go.tz,
- www.tamisemi.go.tz.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**
**04/01/2025**